Jarida Maalum la

# CHANJO

## NA UTAMBUZI WA MIFUGO

www.mifugouvuvi.go.tz | Toleo NO. 6 | Agosti 2025



# Uchanjaji, Utambuzi Mifugo

**Wafikia Asilimia 47.5 Nchi Nzima**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

"Mifugo ni Utajiri,
Chanja na Kuitambua"

# CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO
## yafikia asilimia 47.5 nchi nzima



**Na. Omary Mtamike**

Ikiwa ni takriban mwezi mmoja tangu kuanza kwa utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kitaifa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeweka wazi takwimu za mifugo iliyochanjwa na kutambuliwa hadi Mwezi Agosti 18, 2025 ambapo imefikia milioni **36.2.** Sawa na asilimia **47.46.**

Utekelezaji wa kampeni hiyo ambao ulianzia Wilaya za Longido na Ngorongoro mkoani Arusha Julai 02, 2025 ikiwa ni wiki mbili baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuizindua rasmi Juni 16, 2025 Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

Akizungumza wakati wa kuanza kwa utekelezaji wa kampeni hiyo, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji aliwataka wafugaji wote nchini kutumia fursa hiyo iliyotolewa na Rais Samia kupitia ruzuku ya nusu bei kwa upande wa ng'ombe, mbuzi na kondoo na chanjo ya bila gharama yoyote kwa upande wa kuku wa asili.

"Naomba wataalamu wote wa Mifugo tusikae ofisini twendeni uwandani tukatatue changamoto zote za wafugaji." aliongeza Mhe. Dkt. Kijaji.

Aidha, aliongeza kuwa serikali imeamua kuendesha Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ili kuiwezesha nchi kuuza mifugo na mazao yake kwenye masoko ya nje ambayo awali yalishindwa kupokea kutokana na changamoto ya kutokuwa na ithibati ya usalama wa mifugo na mazao yake ambapo amebainisha kuwa tayari nchi za Misri na Falme za kiarabu zipo tayari kuanza kununua

mifugo hai kutokana na jitihada hizo.

Mara baada ya kuhitimisha zoezi hilo mkoani Arusha, Mhe. Dkt. Kijaji alielekea Wilaya ya Bunda mkoani Mara, ambapo baada ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo alibainisha kuwa Mhe. Rais Samia anakusudia kuidhihirishia dunia utajiri uliopo nchini kupitia Sekta ya Mifugo, hivyo aliwataka wafugaji kuunga mkono jitihada hizo ili mifugo na mazao yake yaendelee kuwa shindani kwenye masoko ya kimataifa.

Ziara ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji iliendelea katika Mkoa wa Simiyu ambapo mbali na kuwapongeza kwa kuitikia wito wa kuchanja mifugo yao alipata fursa ya kusikia ushuhuda wa Mkurugenzi wa kiwanda cha UNION MEAT Bi. Mariam Ng'wani ambaye aliachana na kazi yake ya uanashaeria nchini Ushelisheli na kurejea Tanzania kwa ajili ya kuwekeza kwenye ufugaji.

Ziara hiyo ya Mhe. Dkt. Kijaji iliyolenga kukagua utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa ilifanyika pia katika mikoa ya Geita, Pwani, Morogoro, Tabora na Dodoma ambapo jumla ya mifugo iliyochanjwa na kutambuliwa katika mikoa hiyo hadi sasa imefikia milioni 11.5.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Katikati) akimpa kuku chanjo ya mdondo ikiwa ni ishara ya utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kwa mwaka 2025.**

**“Naomba wataalam wote wa Mifugo tusikae ofisini twendeni uwandani tukatatue changamoto zote za wafugaji”**

**Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji**
**Waziri wa Mifugo na Uvuvi**


**JUMLA YA MIFUGO ILIYOCHANJWA KUFUKIA AGOSTI 18, 2025**

# 36,229,592

Sawa na asilimia **47.46** ya lengo la kuchanja na kutambua mifugo Milioni **76, 329, 100** nchi nzima.



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania | Wizara ya Mifugo na Uvuvi



# TAKWIMU ZA UCHANJAJI NA UTAMBUZI WA MIFUGO 2025

| MKOA | Idadi ya Mifugo iliyochanjwa |
|---|---|
| Tabora | 2,300,226 |
| Singida | 1,908,639 |
| Dodoma | 1,901,429 |
| Geita | 1,790.732 |
| Kagera | 1,767,641 |
| Ruvuma | 1,698,890 |
| Iringa | 1,678,095 |
| Kilimanjaro | 1,584,996 |
| Kigoma | 1,584,996 |
| Mwanza | 1,449,173 |
| Lindi | 1,415,724 |
| Manyara | 1,626.109 |
| Mbeya | 1,280,270 |

| MKOA | Idadi ya Mifugo iliyochanjwa |
|---|---|
| Simiyu | 1,341,095 |
| Arusha | 1,253,357 |
| Songwe | 1,233,565 |
| Rukwa | 1,204,331 |
| Mara | 1,631,018 |
| Njombe | 1,201,979 |
| Shinyanga | 1,179,716 |
| Tanga | 1,311,637 |
| Pwani | 961,185 |
| Mtwara | 928,004 |
| Morogoro | 881,429 |
| Dar es Salaam | 699,428 |
| Katavi | 635,507 |

**MIFUGO**

**JUMLA 36,229,592**

Imechanjwa nchini hadi kufikia Agosti 18, 2025

Sawa na asilimia **47.46** ya lengo la kuchanja na kutambua mifugo Milioni **76, 329, 100** nchi nzima.

https://www.mifugouvuvi.go.tz

wizarayamifugonauvuvi

*" Mifugo ni utajiri , Chanja na Kuitambua"*

*#mifugonauvuviniutajiri*



"Serikali imedhamiria kutokomeza magonjwa ya Mifugo na ndio maana leo tunazindua mpango huu wa chanjo 2025/2029 na hapa kwa dhati kabisa nataka niwapongeze kabisa wafugaji wote Tanzania kwa sababu mmekubali kuchangia nusu na sisi Serikali tutoe nusu kwenye chanjo ya Ng'ombe, Mbuzi na Kondoo"

**MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**Juni 16, 2025**
**Bariadi, Simiyu**



Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo 2025



# Wafugaji watakiwa kupuuza wapotoshaji chanjo ya Mifugo

**Na. Edward Kondela**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti ametoa rai kwa wafugaji nchini kutowasikiliza watu wanaopotosha kuhusu Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kwani inalenga kuboresha mazingira ya mifugo na biashara kimataifa na kwamba haina uhusiano wowote wa kukusanya mapato kwa wafugaji.





Naibu Waziri Mnyeti alibainisha hayo katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga kati ya Julai 4 na 7 mwaka huu, wakati akikagua utekelezaji wa kampeni hiyo, ambapo alisema utoaji wa chanjo na utambuzi wa mifugo hauna uhusiano wowote na wafugaji kudaiwa mapato.

"Natoa wito kwa wafugaji wote, wale wanaopotosha ukweli kuhusu chanjo za mifugo pamoja na habari ya utambuzi, wengine wanasema eti TRA watakuja kutudai, tunazungumzia habari ya kutambua mifugo yetu ili tupate pia idadi ya mifugo iliyopo nchini", alisema Mhe. Mnyeti akiwa katika Kijiji cha Nsola kilichopo Wilaya ya Magu, mkoani Mwanza.

Aliongeza kuwa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo itaiwezesha serikali kujenga majosho kulingana na idadi ya mifugo iliyopo nchini pamoja na kuweka mazingira mazuri ya mifugo yakiwemo maeneo ya machungio na malisho.

Aidha, akiwa katika Shamba la Uzalishaji Mifugo la Serikali Mabuki lililopo Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti, alisema mashamba ya uzalishaji mifugo ya serikali lazima yaachwe yafanye shughuli za serikali kwa ajili ya manufaa ya taifa zima.

Naibu Waziri Mnyeti alisema kuwa mifugo iliyopo katika mashamba ya serikali ni kama mbegu ambazo lazima kuzitunza ili kutoharibu mbegu za asili za mifugo.

"Mashamba ya serikali ni rasilimali za watanzania

wote lazima kulinda kwa pamoja, hizi ng'ombe ni kama mbegu tukiziharibu hizi mbegu ni kwamba tunaharibu kabisa ng'ombe zetu za asili."Alisema Mhe. Mnyeti.

Naibu Waziri Mnyeti alibainisha hayo baada ya taarifa ya kuwepo kwa uvamizi wa mifugo kuingizwa katika Shamba la Uzalishaji Mifugo la Serikali Mabuki kwa ajili ya malisho.

Ng'ombe 20,000 waliovamia Shamba la Mabuki siyo wa wafugaji wa Misungwi isipokuwa wafugaji wa Misungwi wamekuwa siyo waaminifu kwa kukumbatia makundi ya ng'ombe kutoka nje ya Misungwi halafu wanajifanya ni ng'ombe wao." alibainisha Mhe. Mnyeti.

Aliongeza kuwa hayuko tayari kuwatetea wafugaji wanaoingiza mifugo kwenye mashamba ya uzalishaji mifugo ya serikali kwa kuwa hata yeye ni mfugaji lakini anaheshimu maeneo yaliyotengwa na serikali, yakiwemo mashamba ya uzalishaji mifugo ya serikali na kwamba hayuko tayari kupeleka mifugo yake kwenye mashamba hayo bila kufuata utaratibu wa serikali.

Kuhusu utambuzi wa mifugo kwa kutumia hereni za kieletroniki, Mhe. Mnyeti alisema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alielekeza mifugo yote yenye sifa ya kuwekewa hereni lazima itambulike ili kuwezesha pia kufahamu idadi ya mifugo iliyopo nchini.

Aidha, aliwaarifu wafugaji kuwa zoezi la uchanjaji wa mifugo linaenda sambamba na uwekaji wa hereni bure, ambapo hereni hizo pia zitasaidia katika kudhibiti wizi wa mifugo nchini.



Pia, akiwa katika Kijiji cha Mahembe kilichopo Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga mkoani Shinyanga, Mhe. Mnyeti alisema ili mifugo iwe na thamani pamoja na ubora wa kimataifa ni lazima ichanjwe dhidi ya magonjwa, kuoshwa na kutibiwa kwa ajili ya kuondokana na umasikini wa wafugaji na taifa kwa ujumla.

"Unakuta ng'ombe amekondeana kama mfugaji sababu hautaki kumtibu umekaa na ng'ombe analingana kilo na wewe." alisema Mhe. Mnyeti .

Aidha, aliwakumbusha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anawapenda sana wafugaji hadi serikali kulazimika kubeba gharama kwa kutenga Shilingi Bilioni 216 kwa ajili ya zoezi la chanjo na utambuzi wa mifugo nchi nzima.

Nao, baadhi ya wafugaji waliofika kushuhudia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo kwenye ziara ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Alexander Mnyeti, wamesema wamefurahishwa na ruzuku iliyotolewa na serikali ambapo kuku wanachanjwa bure, ng'ombe Shilingi 500 wakati mbuzi na kondoo Shilingi 300.

Wamesema watahakikisha wanafikisha mifugo yao kwa ajili ya kuchanjwa na kufanyiwa utambuzi ili kuwa na mifugo bora dhidi ya magonjwa na kuzuia wizi wa mifugo kwa kufanyiwa utambuzi wa kuwekewa hereni za kieletroniki.
Kampeni hii serikali imetoa ruzuku ya asilimia 100 kwa kuku ambapo watachanjwa bure huku ng'ombe, mbuzi na kondoo ikitoa ruzuku ya asilimia 50.

"
Unakuta ng'ombe amekondeana kama mfugaji sababu hautaki kumtibu umekaa na ng'ombe analingana kilo na wewe.

**Mhe. Alexander Mnyeti**
Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi



# Mifugo Zaidi ya Milioni 70 Kuchanjwa kwenye Kampeni ya Kitaifa

**Na. Hamisi Hussein**

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena amesema mifugo zaidi ya milioni 70 inatarajiwa kuchanjwa nchi nzima kupitia Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa mwaka 2024/2025.

Bi. Meena alisema hayo Julai 6, 2025 wakati wa uhamasishaji wa kampeni hiyo katika Kijiji cha Mpandangindo, Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo aliwahakikishia wafugaji wote nchini kuwa chanjo za mifugo ni salama kwa mifugo yote.

"Kampeni hii ni miaka mitano na hadi Agosti mwaka huu mpango huu utakuwa umekamilika ambapo tutakuwa tumechanja ng'ombe milioni 19, mbuzi na kondoo milioni 17 na kuku milioni 40, chanjo zetu ni salama kwa ajili ya mifugo yetu," alisema Bi. Meena.

Aliwahimiza wafugaji wote nchini kushiriki kikamilifu katika uchanjaji huo kwa kutoa mifugo yao na kubainisha kuwa katika mwaka 2024/2025 inatarajiwa kukamilika Mwezi Agosti mwaka huu, lengo likiwa ni kuikinga mifugo dhidi ya magonjwa yanayoathiri biashara ya mifugo na mazao yake.

> **"Kampeni hii ni ya miaka mitano na hadi Agosti mwaka huu mpango huu utakuwa umekamilika ambapo tutakuwa tumechanja ng'ombe milioni 19, mbuzi na kondoo milioni 17 na kuku milioni 40, chanjo zetu ni salama kwa ajili ya mifugo yetu,"**
>
> Bi. Agnes Meena
> Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi



Kwa upande wake Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Bw. Jumanne Mwankhoo alisema mkoa huo utaendelea kumilikisha ardhi kwa wafugaji ili kuondoa migogoro inayojitokeza baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

Kwa upande wake Katibu wa Chama cha Wafugaji Tanzania Kanda ya Kusini (CCWT) Bi. Prisca Kaponda aliwahimiza wafugaji wote wa kanda hiyo kushirki kikamilifu katika kampeni hiyo kwa kuwa chanjo hizo ni salama na zimezalishwa hapa nchini.

## Wataalamu, Maofisa Wahadharishwa Kujinufaisha Chanjo ya Mifugo

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imetoa onyo kwa maofisa na wataalamu wanaotekeleza Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, kutotumia vifaa vya chanjo kujinufaisha kibiashara na badala yake vitumike kuchanja mifugo kama ilivyokusudiwa na serikali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Bi. Agnes Meena akiwa kwenye ziara yake ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo kwa Mkoa wa Lindi, aliwahamasisha wafugaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Manispaa ya Lindi, kisha kutoa tahadhari kwa maafisa na wataalamu kutotumia chanjo na vifaa vyake kujinufaisha kibiashara.

Alisema serikali imechangia nusu ya gharama kwa chanjo ya mifugo kote nchini, hivyo wataalamu wasitumie vifaa vya chanjo kwa manufaa yao wenyewe bali vitumike kama ilivyokusudiwa na serikali.

"Nipende kuwahimiza viongozi na wataalamu kuhakikisha kuwa hizo chanjo tulizotoa, kila kitu kitumike kama ilivyopangwa, tusianze biashara, kuku wote watachanjwa bure lakini ng'ombe, mbuzi na kondoo mtachangia kidogo," alisema Bi. Meena.



Kwa upande wake, daktari wa mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Daniel Mdetele alisema baada ya kutambua magonjwa yanayoathiri mifugo na mazao katika masoko ya kimataifa, wizara ilianisha magonjwa 13 ya kipaumbele na kuchukua hatua za kukabiliana nayo ikiwemo utoaji wa chanjo kwa mifugo yote nchini.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa chanjo daktari wa mifugo wa Wilaya ya Kilwa, Dkt. Nyalekwa Mashimo alisema wilaya hiyo ilipokea chanjo za mdondo wa kuku 300,000 na hadi Juni 30, mwaka huu kuku 30,000 zilichanjwa ikiwa ni sawa na asilimia 10 ya chanjo ya kuku iliyopokelewa.

## Chanjo ya Mifugo Iendane na Ufugaji wa Kisasa

Akiwa katika Halmashauri ya Masasi Mji mkoani Mtwara, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bi. Agnes Meena, alitoa rai kwa wafugaji kuongeza tija ya mifugo yao kwa kutumia mbegu bora zitakazowanufaisha kiuchumi ili kuongeza pato la taifa kupitia Sekta ya Mifugo.





Akizungumza na wafugaji wakati wa uhamasishaji wa kupitia Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa Mkoa wa Mtwara Bi. Meena alisema wafugaji wanapaswa kujifunza na kutumia mbegu bora za mifugo ili kujiongezea kipato.

"Kujifunza sio hadi uende nje ya nchi hata hapa ndani kwetu, nendeni mkajifunze kule Kilwa ili mpate mbegu bora zitakazowezesha kuongeza mifugo itakayowaongezea kipato na kuwa matajiri", alifafanua Bi. Meena.

Kuhusu mpango wa chanjo unaoendelea kutekelezwa nchini Bi. Meena alisema serikali itafanya ufuatiliaji wa kampeni hiyo nchi nzima ili kutimiza lengo la kudhibiti magonjwa ya mifugo jambo litakalosaidia kuimarisha biashara ya mifugo na mazao yake katika masoko ya ndani na kimataifa.

"Tunataka kuwafanya wafugaji wetu kuwa matajiri kwa hiyo kampeni hii ya chanjo na utambuzi kote nchini tutaifuatilia ili tutimize malengo tuliyojiwekea", aliongeza Bi. Meena.

Kwa upande wake Katibu Tawala wa Mkoa wa Mtwara Bi. Bahati Geuzye alisema zaidi ya dozi milioni 1.5 za mdondo wa Kuku, dozi 335,000 za sotoka ya mbuzi na kondoo na dozi 85,000 za homa ya mapafu ya ng'ombe zitatumika kudhibiti magonjwa ya mifugo.

***Tunataka kuwafanya wafugaji wetu kuwa matajiri kwa hiyo kampeni hii ya Chanjo na Utambuzi kote nchini tutaifuatilia ili tutimize malengo tuliyojiwekea***

Bi. Agnes Meena
Katibu Mkuu - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

# SERIKALI YASONGA MBELE KAMPENI YA KITAIFA YA CHANJO YA MIFUGO



## Na Daudi Nyingo

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imeendelea kutekeleza kwa kasi Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo, mpango wa miaka mitano uliobuniwa ili kulinda afya ya mifugo, kuongeza tija ya uzalishaji na kufungua fursa za masoko ya ndani na nje. Kampeni hiyo, iliyoanzishwa na kuzinduliwa rasmi Juni 16, 2025, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, mjini Bariadi, Simiyu, inalenga kuchanja na kutambua mamilioni ya mifugo kote nchini.

Katika ziara zake kwenye mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. Edwin Mhede, pamoja na viongozi wengine waandamizi wa wizara, wameongoza moja kwa moja zoezi hilo na kujionea mwitikio chanya wa wafugaji.

**Iringa: Wafugaji Wajitokeza kwa Wingi**

Julai 3, 2025, akiwa mkoani Iringa, Dkt. Mhede alizindua zoezi hilo kwa kutembelea Shamba la Kibebe na Kijiji cha Kalenga, ambako jumla ya ng'ombe 1,223 walitambuliwa na kuchanjwa siku hiyo pekee. Alisema mkoa unalenga kuchanja zaidi ya ng'ombe 400,000. Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Kheri James, alisisitiza kuwa afya ya mifugo ni msingi wa ustawi wa jamii na kwamba mkoa umejipanga kuhakikisha kila halmashauri inashiriki kikamilifu. Wafugaji walifurahia punguzo la gharama ya chanjo kutoka Sh 1,000 hadi Sh 500 kwa kila ng'ombe.

**Njombe: Chanjo Bure kwa Kuku**

Siku iliyofuata, Julai 4, 2025, mkoani Njombe, Dkt. Mhede alithibitisha kuwa chanjo zote zimesambazwa na wataalamu waliopatiwa mafunzo wapo kazini. Mkoa unalenga kuchanja ng'ombe 240,000 na kuku zaidi ya milioni 1.3. Afisa Mifugo wa Mkoa, Bw. Nicolas Buji, alisema chanjo ya homa ya mapafu kwa ng'ombe inagharimu Sh 500 kwa mfugaji huku serikali ikichangia zaidi

# Utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo 2025



ya nusu ya gharama, na chanjo ya kuku ikitolewa bure. Meneja wa Shamba la Kitulo, Bw. Joseph Mlelwa, aliwataka wafugaji kote nchini kuitikia wito huo wa kitaifa.

### Mbeya: Mkakati Dhidi ya Magonjwa 11 Makuu

Julai 5, 2025, mkoani Mbeya, Dkt. Nazaeli Madalla, akimwakilisha Dkt. Mhede, alisema serikali imetambua magonjwa 11 makuu yanayopunguza tija, ikiwemo homa ya mapafu kwa ng'ombe, sotoka kwa mbuzi na kondoo, na magonjwa ya kuku kama kideri na ndui.

Mkoa wa Mbeya una mifugo milioni 3.3, na umepokea chanjo zote pamoja na vifaa vya utambuzi wa kidijitali. Wataalamu walisema chanjo zitasaidia kudhibiti magonjwa na kuimarisha usajili wa mifugo, jambo litakalosaidia pia kutatua migogoro ya ardhi.

### Songwe: Uzinduzi wa Programu ya Kimkoa

Julai 7, 2025, mkoani Songwe, Dkt. Mhede alizindua rasmi programu hiyo ya kimkoa katika Kijiji cha Ndanga, Wilaya ya Songwe, akisema zaidi ya ng'ombe 479,800 na kuku milioni 2.3 watanufaika.

Katika siku ya kwanza, zaidi ya ng'ombe 1,500 walichanjwa na kutambuliwa. Alisisitiza kuwa mifugo itakayochanjwa pia itavishwa hereni za kielektroniki kwa ajili ya usalama na utambulisho. Wafugaji walipongeza mpango huo, wakisema utasaidia kupunguza magonjwa na kuongeza thamani ya mifugo yao.

### Rukwa: Onyo kwa Watumishi Wanaokiuka Mwongozo

Julai 8, 2025, akiwa katika Ranchi ya Taifa ya Kalambo, mkoani Rukwa, Dkt. Mhede alitoa onyo kali kwa watumishi watakaojaribu kuwatoza wafugaji fedha kinyume na muongozo, akisisitiza kuwa serikali imegharamia asilimia 100 ya shughuli zote za chanjo na utambuzi. Mkoa wa Rukwa unatarajia kuchanja zaidi ya ng'ombe 400,000 pamoja na mbuzi, kondoo na kuku.

Katibu Tawala wa Mkoa, Robert Makungu, alisema hatua hiyo ni mkakati wa kupunguza vifo vya mifugo na kuboresha maisha ya wafugaji. Wafugaji walieleza kufurahia pia utoaji wa hereni za kielektroniki bure, ambazo awali ziligharimu Sh 1,750.

**Faida na Malengo ya chanjo na utambuzi**

1. Chanjo ya Mifugo imelenga kulinda afya ya mifugo.

2. Kuongeza tija, kufungua masoko ya kimataifa kupitia diplomasia ya uchumi, na kuboresha kipato cha wafugaji.

3. Kupunguza gharama kwa ruzuku ya serikali na kutoa chanjo bure kwa baadhi ya mifugo.

kampeni hii imepokelewa kwa mwitikio chanya kote nchini. Wafugaji na viongozi wa mikoa wamesema wanatarajia kuona ongezeko la uzalishaji, usalama wa chakula, na kipato cha familia kupitia sekta ya mifugo.



# Chanjo na Utambuzi wa Mifugo ni Kinga na Tiba bora kwa Mifugo

## Na. Stanley Brayton

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza rasmi mpango kabambe wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, yenye lengo la kuboresha afya ya mifugo nchini na kufungua soko la kimataifa kwa mazao yatokanayo na mifugo.

Katika kuhakikisha kampeni hiyo inatekelezwa kikamilifu, baadhi ya viongozi wa wizara pamoja na taasisi zilizo chini yake wakiongozwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, walifika katika baadhi ya mikoa kufuatilia utekelezaji wa kampeni hiyo iliyozinduliwa Juni 16, 2025 mkoani Simiyu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Prof. Erick Komba akiwa katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Tanga kukagua utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, alisema mifugo inakabiliwa na changamoto nyingi hususan ya magonjwa ambayo mengine husababisha vifo na kukosesha taifa soko la kimataifa kutokana na mifugo kutofikia viwango vinavyohitajika vya kudhibiti magonjwa.



Katika hatua ya awali, Prof. Komba alipatiwa taarifa kuwa takriban mifugo 3,010 ilikuwa imechanjwa katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Tanga ili kuboresha na kuletamabadiliko makubwa katika Sekta ya Mifugo na kuondoa vikwazo ambavyo vimekuwa vikizuia mifugo na mazao yake kuuzwa katika soko la kimataifa.

Prof. Komba alifafanua kuwa idadi ya ng'ombe waliokuwa wamechanjwa walikuwa 1,951, mbuzi 549, Kondoo 265 na Kuku 245.

"Mkoani Manyara hadi sasa walishachanjwa ng'ombe 420, Mbuzi 283, Kondoo 121, kuku 30 na mkoani Kilimanjaro mifugo iliyochanjwa ni ng'ombe 991, mbuzi 206, kondoo 94, kuku 15, hali kadhalika mkoani



ni ng'ombe 540, mbuzi 60, kondoo 50 na kuku 200." alisema Prof. Komba.

Kwa upande wake, Katibu Tawala Wilaya ya Babati, Bw. Thobias Abwaro akimwakilisha mkuu wa wilaya hiyo katika zoezi la uhamasishaji na utoaji wa chanjo za mifugo mkoani Manyara, alisema kwa muda mrefu uchanjaji wa mifugo ulikuwa ukifanyika kidogo katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa, mashamba makubwa na mfugaji mmoja mmoja bila kuwa na uratibu wa pamoja ambao hauwezi kutokomeza magonjwa ya mifugo, kwa kuwa ili kutokomeza magonjwa hayo inabidi kuchanja mifugo angalau kwa asilimia 70.

Serikali imeazimia kutokomeza magonjwa matano ya mifugo yaliyowekewa kipaumbele ili kuboresha na kuondoa vifo vya mifugo dhidi ya ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku.

Akiweka wazi aina za chanjo zinazotolewa katika Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo, Kaimu Msajili wa Baraza la Veterinari Tanzania (VCT), Dkt. Obed Nyasebwa, alizitaja kuwa ni homa ya mapafu ya ng'ombe, sotoka ya mbuzi na kondoo pamoja na magonjwa ya kuku ya mdondo, mafua na ndui.

Kuhusu utekelezaji wa kampeni hiyo, unaanza na mfugaji namba moja nchini ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia serikali kugharamia Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa kwa miaka mitano kuanzia 2025 hadi 2029 kwa shilingi shilingi bilioni 216 na kutoa ruzuku ya chanjo bure za kuku, na kutoa pungufu ya asilimia 50 kwa chanjo za ng'ombe, mbuzi na kondoo, ambapo mfugaji atalipia shilingi 500 kwa ng'ombe na shilingi 300 kwa mbuzi na kondoo.

Kutokana na hatua hii ya Serikali ya Awamu ya Sita, Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa inatekelezwa katika mikoa na halmashauri zote nchini, ambapo katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni mkoani Tanga, daktari wa mifugo wa halmashauri hiyo Dkt. Key Amiri alisema wamepata vifaa vyote vya uchanjaji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ikiwemo dozi 100,000 za chanjo ya homa ya mapafu ya ng'ombe, dozi 240,000 za chanjo ya ugonjwa wa sotoka, dozi 240,000 na chanjo ya tatu moja kwa ajili ya kuku ambayo inatibu ndui na mafua pamoja na dozi 170,000 za kideli, hereni za utambuzi na vifaa vingine.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, katika Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa katika mkoa huo, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Mhe. Godfrey Mnzava, alisema halmashauri za wilaya, zilishapokea chanjo zote ambapo mifugo 3,405,500 iliwekewa lengo kwa ajili ya kuchanjwa na kutambuliwa mkoani hapo ambapo ng'ombe ni 492,700, mbuzi na kondoo 1,212,800 na kuku 1,700,000.

Mhe. Mnzava alibainisha kuwa utoaji wa chanjo unaoenda sambamba na utambuzi wa mifugo, utaongeza chachu ya kufuga kisasa na kuboresha maisha ya wafugaji kupitia masoko ya mifugo na mazao yake ambapo hereni za kieletroniki zitasaidia katika kuhifadhi taarifa za mifugo kwenye vishikwambi.

Kaimu Mwenyekiti wa Chama Cha Wafugaji Wilaya ya Handeni (CCWT) mkoani Tanga, Bw. Clement Soba alisema Serikali ya Awamu ya Sita imewatambua wafugaji na kutoa ishara kuwa Sekta ya Mifugo ni muhimu, hivyo wafugaji wa Wilaya ya Handeni wameamua kujitokeza kwa wingi ili kuchanja mifugo kutokomeza magonjwa na kuiwezesha sekta hiyo kukua kiuchumi kwa kuwa mifugo inapochanjwa na kutambuliwa inakuwa salama na kulinda afya ya mlaji.

Penye nia pana njia, hii inakuja baada ya wafugaji kufungua masikio yao na kuamua kuchanja mifugo yao ili kuiona fursa ya kibiashara ambayo inaletwa na ufugaji wa kisasa.

Katika utekelezaji wa kampeni hii, wafugaji na viongozi wa serikali walimshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ruzuku ya chanjo za mifugo na utambuzi kitaifa.

Akihitimisha ziara ya kufuatilia utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Tanga, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI), Prof. Erick Komba alisema mifugo inaathiriwa sana na magonjwa mbalimbali ambayo yanapelekea vifo vya mifugo hivyo chanjo ni muhimu ili kudhibiti magonjwa.

Pia, alisema mbali na vifo vya mifugo mazao yake yamekuwa yakikosa soko la kimataifa kutokana na kukosa viwango vinavyohitajika katika mataifa mbalimbali hali iliyosababisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuridhia serikali kutoa ruzuku katika utoaji wa chanjo na kuitambua mifugo kwa njia ya hereni za kieletroniki.

Vilevile, Prof. Komba alisema kuwa imani yake ni kwamba Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa itafanikiwa kwa asilimia mia moja na kuimarisha mifugo na hatimaye kuwa na mazao bora zaidi.

Prof. Komba aliwataka wafugaji kujitokeza kwa wingi katika kuchanja mifugo yao ili kutokomeza magonjwa kwani kampeni hii ni fursa adhimu kwa wafugaji.











# Mifugo ni Utajiri, Chanja na Kuitambua

# TANZANIA YAANZA RASMI UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA CHANJO NA UTAMBUZI WA MIFUGO

- *Serikali yatoa nafuu ya kuchanja na kutambua mifugo*
- *Mifugo zaidi ya milioni tatu kuchanjwa, kutambuliwa mikoa ya Kigoma, Katavi na Singida.*



## Na Chiku Makwai

Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeanza rasmi utekelezaji wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Singida ambapo mifugo zaidi ya 3,000 imechanjwa na kutambuliwa katika wilaya ya Uvinza, Mpimbwe na Iramba.

Katika kampeni hii, zaidi ya mifugo milioni tatu inatarajiwa kuchanjwa na kutambuliwa katika mikoa hiyo kwa lengo la kuimarisha afya ya mifugo ili kukidhi vigezo na kupata ithibati kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi.

Itakumbukwa kwamba Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali ya Awamu wa Sita iliyo chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ilitangaza rasmi kuunga mkono Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa na kukubali kutoa ruzuku kwa uchanjaji na utambuzi wa mifugo hiyo. Juni 16, 2025 katika Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, Mhe. Rais. Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua kampeni hiyo na kuelekeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kutekeleza kampeni hii katika mikoa yote nchini.

“Naunga mkono kampeni hii na nimekubali kwamba serikali ibebe nusu ya gharama za chanjo lakini nimefurahi kusikia kwa kuku chanjo ni bure maana najua ufugaji kuku ni mradi wa akinamama wengi.” Kauli

ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa mifugo kitaifa uliofanyika Mkoani Simiyu Juni 16, 2025.

Akishiriki katika kampeni hii Julai 3, 2025 katika Wilaya ya Uvinza, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Mhe. Balozi Simoni Sirro alisema ni vyema wafugaji wajifunze kufuga kisasa ili wanufaike na mifugo yao ikiwemo kuipatia chanjo dhidi ya magonjwa.

Aidha Balozi Sirro alisema kuwa takriban mifugo zaidi ya laki 300,000 inatarajiwa kuchanjwa mkoani humo ambapo aliwasihi wafugaji kujitokeza na kushiriki katika kampeni hiyo na kuhakikisha wanakuwa na mifugo yenye afya wakati wote ili kulinda afya za walaji.

Naye Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe mkoani Katavi Bi. Shamimu Mwariko alisema kampeni ya chanjo na utambuzi wa mifugo itawasaidia watendaji wote nchini kuweza kuandaa mpango bora wa kutoa huduma sahihi kwa wafugaji na kusimamia mifugo katika maeneo yao.

Aidha, Bi. Mwariko aliongeza kuwa katika Mkoa wa Katavi mifugo zaidi ya 800,000 inatarajiwa kuchanjwa na kutambuliwa ambapo aliwahimiza wafugaji wote mkoani humo kujitokeza kuchanja na kutambua mifugo ili waweze kunufaika na kampeni hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji, Julai 8, 2025 katika Kijiji cha Makunda wilayani Iramba mkoa wa Singida, Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA) Dkt. Pius Mwambene, alisema Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, ambayo ilizinduliwa June 16, 2025 na Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan itaongeza tija kwa wafugaji kote nchini hivyo wanapaswa kuizingatia.

Adha, Dkt. Mwambene alisema kwa upande wa Mkoa wa Singida zaidi ya mifugo milioni 1.9 inatarajiwa kuchanjwa na kutambuliwa, hivyo wafugaji watachanja mifugo yao kwa bei ya ruzuku baada ya serikali kutenga shilingi bilioni 216 kwa ajili ya kuwezesha kampeni hiyo, kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo.

Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa Mifugo Kitaifa, imelenga kudhibiti magonjwa ya homa ya mapafu kwa ng'ombe (CBPP), sotoka (PPR) dhidi ya mbuzi na kondoo pamoja na magonjwa dhidi ya kuku; mdondo (ND), ndui na mafua.

Ili kutokomeza magonjwa hayo na kukidhi vigezo vya kupata ithibati ya soko la kimataifa, serikali imeamua kuanzisha Kampeni ya Chanjo na Utambuzi wa mifugo nchini kwa mujibu wa maelekezo ya kisayansi yanayosimamiwa na Shirika la Afya ya Wanyama Duniani (WOAH).



# MATUKIO KATIKA PICHA









# MATUKIO KATIKA PICHA









# MATUKIO KATIKA PICHA









# BODI YA UHARIRI

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mbaraka Kambona | - | Mwenyekiti |
| 2. Edward Kondela | - | Mhariri Mkuu |
| 3. Elibariki Mafole | - | Mhariri |
| 4. Hamisi Hussein | - | Msanifu Kurasa |
| 5. Omary Mtamike | - | Mwandishi |
| 6. Daudi Nyingo | - | Mwandishi |
| 7. Stanlay Brayton | - | Mwandishi |
| 8. Chiku Makwai | - | Mwandishi |


## TUFUATILIE

**Kwenye Mitandao ya Kijamii kwa jina la Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupata taarifa zetu**

www.mifugouvuvi.go.tz

# Jarida Maalum la Chanjo na Utambuzi wa Mifugo - 2025

Wizara ya Mifugo na Uvuvi
Mtaa wa Ulinzi, Mji wa Serikali
Mtumba S.L.P 2847, Dodoma, Tanzania

Simu: **+255 26 2322610**
**Barua Pepe : barua@mifugo.go.tz**